

Idadi ya wanambuzi na wanakondoo kwa kila nyumba

Ukubwa wa nyumba na umri wa wanambuzi, wanakondoo na ndama utaathiri idadi itakayowekwa kwa kila nyumba. Nyumba wastani ya upana wa mita 1 hutoshea watoto 7 wa miezi 3.

Faida za kutumia nyumba za Risayoni

- Kazi ya kuwashughulikia watoto hupunguzwa na hasa kazi ya kusafisha nyumba mara kwa mara hupungua ambayo mara nyingi hufanywa na wanawake na watoto.
- Huokoa miti ya nyika kwani ni idadi kidogo tu inayotumika.
- Nyumba ikitunzwa vizuri inawza kudumu miaka 3.
- Hupunguza athari za nzi chawa na kupe pamoja na wavamizi wengine na gharama ya madawa pia hupunguzwa.
- Kwa wafugaji wa kuhamahama, punda waweza kutumiwa kubeba nyumba hizo kutoka mahali pamoja hadi pengine.
- Vifo vya wanambuzi, wanakondoo hupungua kutoka asilimia 35 hadi 10.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Barua pepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishaji:

Lengarite M. na Kuria G.S.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Marsabit

S.L.P. 147, Marsabit -60500

Simu: 069-2040/2220

Nukulishi: 069-2220

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 53 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Nyumba za kuhamishwa za Risayoni kwa wanambuzi na wanakondoo



Utangulizi

Nyumba mbaya katika maeneo za watu wa kuhama hama ni chanzo kikubwa cha maafa ya wanambuzi na wanakondoo.

Nyumba za kawaida hujengwa kwa miti inowapelekea kupata joto jingi, kuvamiwa na hata kupatwa na wadudu wa magonjwa.

Kibada cha nyumba za kawaida ni nyumba aina ya *Risayoni* ya kuhamishwa ya kiwango bora na faida nyingi.

Jinsi ya kutengeneza nyumba ya *Risayoni*

Huwa na umbo la nusu mwezi na huwa ya ukubwa unaotofautiana (ndogo, wastani na kubwa).


Asilia

- Mtiti yenye nguvu ya mita 1.5 hadi 3 kwa urefu na upana wa kidole cha mkono nyaya za kufunganisha sawa na zile zinazotumika katika kuunga mikufu au maganda ya miti.
- Miti inayopatikana humu ambayo inaweza kukunjwa iwe nusu mviringo bila kuvunjika kama vile *Grevillea*, *Duom Palm* na *Commiphora*

Hatua ya kwanza: Fremu ya kimsingi

Tengeneza fremu ya msingi kwa kuunga miti miwili ya upana wa kidole pamoja na kutunga nusu mviringo.


lunganisha miti ile miwili pamoja kwa kutumia nyaya za kuunganisha.



Fremu ya msingi

Hatua ya pili: Umbo la ufa


- Kunja miti ya urefu wa 1.5 hadi 3 ili kuunda nusu mviringo. Unganisha sehemu za mwisho na zile za fremu ya msingi.
- Miti iliyokunjwa upande wa juu sharti ipitane na iunganishwe pamoja kwa kutumia nyaya au maganda laini ya miti.



Umbo la paa

Hatua ya tatu: Kumaliza ujenzi

Tumia karatasi ya nailoni, kinyesi cha ng'ombe, matawi ya *Duom* au vipande vya nguo kuukuu kuingia ile fremu. Sharti nyumba hiyo iwe na dirisha za kutosha ili kuruhusu hewa safi kuingia na mlango kutoka kwa miti au mabati makuukuu.



Vipande vikavu ndani ya magunia?

Usafi na kutunza

- Iweke nyumba mahali tofauti kila siku.
- Baada ya wanambuzi ama wanakondoo kukua na kuiacha nyumba, ipindue juu-chini ili kuangamiza kupe, chawa na nzi kwa joto la jua ili kuifanya nyumba kukaa bila wadudu.
- Baada ya ya kuwaachisha wanambuzi, wanakondoo na ndama, ihifadhi nyumba hii kwa matumizi ya baadaye. Iweke juu mbali na mchanga ili kuzuia kuathiriwa na mchwa au kuharibiwa na jua kali. Ikarabati mara kwa mara maana watoto huiharibu.